# UJUMBE WA MWAKA WA 2019

MUNGU AITWE MUNGU

ndani ya vyote vyenye aliumba.

MUNGU AITWE MUNGU

juu mbinguni na hapa duniani.

MUNGU AITWE MUNGU

ndani ya Cherubim na Seraphim wote.

Mama MARIA

aongoze Cherubim na Seraphim,

aongoze wa Malaika na Watakatifu wote juu mbinguni wamutukuze MUNGU

kwa niaba yetu sisi wanadamu.

MUNGU  muumba wetu anajaa uwezo.

Asifiwe sana.

Yeye ndiye muumbaji wa vyote vyenye tunaona na vyenye bado hatujaona.

Jina lake litukuzwe sana.

MUNGU BABA  Yeye ndiye ALPHA NA OMEGA.

Wote wenye wako mbinguni wamutukuze milele na milele. Amina.

Vyote vyenye aliumba: mwezi na jua, nyota na bahari, miti na mimea, minyama na ndege, na sisi wote wanadamu, tumutukuze Muumba wetu.

Siku baada ya siku tuende kwa magoti kwa ajili ya kumupea sifa, shangwe na vigelegele.

Ni mwema sana.

Ni wa uwezo sana.

Jina lake litukuzwe.

(Zaburi 115,  Zaburi 118, Zaburi 123, Zaburi  124, Zaburi 131, Zaburi 135, Zaburi 136, Zaburi 138, Zaburi 139, Zaburi 145, Zaburi 146, Zaburi 148).

**ZABURI 148: Mbingu na dunia zimusifu Bwana**

**Aleluya!**

**Msifuni Bwana toka mbinguni**
**Msifuni mahali pa juu!**
**Msifuni, enyi malaika wake wote,**
**msifuni, enyi majeshi yake yote.**

**Msifuni, enyi jua na mwezi,**
**msifuni, enyi nyota zote zenye kun'gara.**
**Msifuni, enyi mbingu za juu**
**na maji yaliyo juu ya anga.**

**Vyote visifu jina la Bwana,**
**maana Yeye aliamuru, vikaumbwa.**
**Akaviweka hata milele na milele,**
**akatoa amri isiyovunjika.**

**Msifuni Bwana toka duniani;**
**enyi majoka na vilindi vyote vya bahari,**
**enyi moto na mvua ya mawe, seluji na ukungu,**
**na upepo wa tufani unaotimiza neon lake;**
**enyi milima na vilima vyote,**
**na miti ya matunda na mierezi yote.**

**Enyi wanyama wa porini na wanyama wa kufugwa,**
**na wenye kutambaa chini na ndege zenye mabawa;**
**enyi wafalme wa dunia na mataifa yote,**
**enyi wakuu na watawala wote wa dunia;**
**enyi, vijana waume na wabinti,**
**enyi wazee pamoja na watoto.**

**Wote walisifu jina la Bwana,**
**maana jina lake ni kubwa peke yake;**
**utukufu wake wapita dunia na mbingu,**
**Amekuza nguvu ya taifa lake.**
**ndiyo masifu ya waamini wake wote,**
**ya wana wa Israeli, taifa lenye kumjongea!**

**Aleluya!**

MUNGU NI MUNGU

MUNGU NI WA UWEZO

MUNGU NI WA MAAJABU

Hana mwanzo wala mwisho.

Atukuzwe sana.

Ainuliwe sana.

Na asifiwe sana.

Sisi wote wanadamu wa Afrika, wa Uropa, wa Amerika, wa Asia, wakusoma na wasio wakusoma, watajiri au masikini, watoto au wakubwa, tunyenyekee mbele yake na mioyo zetu zote. Tunyenyekee mbele ya utukufu wake. Tumupe sifa, shangwe na vigelegele. Anastahili siku zote. Na ndiye Yeye muumba wetu.

Soma Zaburi 92, Zaburi 93, Zaburi 95, Zaburi 96, Zaburi 97, Zaburi 98, Zaburi 99, Zaburi 100

Wazazi wangu wapendwa, kaka zangu na dada zangu, pale popote mulipo kwa dunia, mumuogope MUNGU, mumusifu MUNGU na mumutukuze MUNGU. Ndiyo shauri alituumba. (Matayo 6:20-34).

Wapendwa wa MUNGU, nyinyi wote na nyumba zenu, tumuogope MUNGU na tumutukuze MUNGU siku zote za maisha yetu.

Ndiyo tutakuja kubarikiwa.

Watoto wetu watabarikiwa.

Wazazi tutabarikiwa.

Kazi za mikono zetu zitabarikiwa.

Masomo ya watoto itabarikiwa.

Maisha ya kila mmoja wetu itabarikiwa.

Jinsi wazazi wetu katika imani (Ibrahim, Yakobo, Eliya na wengineo) walivyobarikiwa na sisi ndiyo hivyo tutabarikiwa.

**Kumuogopa MUNGU na kumutukuza MUNGU kunaleta baraka.**

Ibrahim alimuogopa MUNGU na alibarikiwa.

Yakobo alimuogopa MUNGU na alibarikiwa.

Eliya alimuogopa MUNGU na aliwafundisha watu wamuogope MUNGU, alibarikiwa na wenye alifundisha nao walibarikiwa.

Yonah alitumwa na MUNGU aende Ninive. Wa Ninive walipona kifo kwa shauri walimuogopa MUNGU.  (Yonah 3:1-10)

Judith alimuogopa MUNGU akabarikiwa, na akafundisha wa Israeli kumuogopa MUNGU.

Na nyinyi wazazi wangu wapendwa na ndugu zangu, tunastahili tufundishe wengine, tufundishe watoto wetu wote, kumuogopa MUNGU na kunyenyekea mbele yake.

Nawaomba tena nawasihi, musome kitabu cha Ukumbusho 6:1-25. MUNGU wetu na muumba wetu anatuambia tusimupime, tusimujaribu, tusicheze na yeye na tusikuwe walegevu katika sala.

Nitaongeza kuwaomba musome kwa makini kitabu cha Ukumbusho 5:1-33. Kitawasaidia sana kwa kuongeza kumuogopa MUNGU na kushika amri zake.

Wazazi wangu wapendwa, wa karibu na wa mbali, wa continent zote, nawasihi sana tena nawaomba na unyenyekevu wote, mupate na wakati musome kitabu cha Yobu kwa utulivu:

Yobu 38 yote,

Yobu 39 yote,

Yobu 40 yote,

Yobu 41 yote

na Yobu 42 yote.

Kitabu hiki kitawasaidia MUNGU wetu na muumba wetu kumukamata na heshima yote na unyenyekevu wote siku zote za maisha yenu.  Na jamaa zetu zitabarikiwa. Watoto wetu watabarikiwa.  Kizazi na kizazi kitabarikiwa. Amina.

Wazazi wangu wapendwa, ndugu na dada zangu wapendwa wa ulimwengu mzima popote mulipo, kuanzia kwa Noeli hii mpaka kwa Noeli zote zenye MUNGU atawapatia hapa dunuani, nawaomba na tena nawasihi, MUNGU mumuombe (namna Mfalme Solomoni alimuomba) awapatie zawadi ya hekima, na pia awapatie vipaji 7 vya MUNGU ROHO MTAKATIFU.

***Kwa sababu katika Injili ya Yohana Yesu aliwaambia Mitume ati alikuwa na mengi ya kuwaambia lakini hawataviweza bila kuongozwa na ROHO MTAKATIFU, na akaongeza akawaambia MUNGU ROHO MTAKATIFU akija atawafafanulia vyote na atawaongoza kujua vyote.***

Na sisi wanadamu tunastahili tuongozwe na ROHO MTAKATIFU katika maisha yetu yote hapa duniani, katika milima na mabonde ya hii dunia, katika mateso na furaha zenye zimejaa ndani ya dunia hii.

Wazazi wangu wapendwa, na dada zangu na ndugu zangu wapendwa, pia nitawaomba musome wa Galatia 5:1-26, itawaonyesha vizuri baraka  Mtume Paulo zenye aliwaambia wa Galatia zenye tunapata wakati tunaongozwa na ROHO MTAKATIFU.  Aliwaambia wa Galatia, na sisi wa leo anatuambia, **tuongozwe na ROHO MTAKATIFU**.  Amina.

Nitawaomba wazazi wangu wapendwa, kwa unyenyekevu wote na heshima yote, na kuwasihi wote musome kitabu cha Hekima:

Hekima 6 yote,

Hekima 7 yote,

Hekima 8 yote,

na Hekima 9:1-18 kwenye kuko sala ya kila siku yenye tunastahili tuisome kile siku ya maisha yetu yote.

Watoto wenu muwaambie waisome, na nyinyi wazazu wangu wapendwa, muisome kila siku, siku zote za maisha yenu.

Kupitia kwa hiyo sala ya kumuogopa MUNGU, MUNGU atatubariki na hekima yake, na vipaji 7 vya ROHO MTAKATIFU.  Amina.

Wakristu wapendwa, na wadada zangu na wandugu zangu wapendwa, ninawasihi na kwa unyenyekevu wote ninawaomba pia musome kitabu cha Busara ya Sira 1:1-29 na 2:1-18. Kitawaonyesha utukuvu wa MUNGU na hekima yake kusudi mumuogope MUNGU.

Katika sala zangu nitawaombea sana MUNGU awajalie zawadi kuu ya kumuogopa MUNGU na kumutukuza MUNGU, na kushika amri zake kumi siku zote zenye ataturuhusu tuishi hapa duniani. Amen.

Kupitia kwa uongozi wa ROHO MTAKATIFU tutapata baraka ajabu, na familia zetu zitabarikiwa. Kazi za mikono zetu zitabarikiwa, na MUNGU atafungua milango za mbinguni ateremushe baraka juu ya baraka. Wema na ukuu wake utatuadamana siku za maisha yetu zote.

Wazazi wangu wapendwa tutamani kuliko kutamani uongozi wa MUNGU ROHO MTAKATIFU katika shughuli zetu zote za kiroho na za kimwili. Tutamupendaza sana MUNGU BABA na MUNGU MWANA.

Wazazi wangu wapendwa pale popote mulipo, mushike na utaratibu ajabu amri zote za MUNGU. Na mufunguke macho musirudie kutumika siku ya MUNGU. Siku ya MUNGU ni siku yenye MUNGU alijiteulia yeye mwenyewe na akaibariki na akaifanya takatifu.

Mutasoma katika kitabu cha Mwanzo 1:1-31.

Pia mutasoma kuhusu Dimanche (Sunday) kwa kitabu cha Hesabu 15:32-36.

Na kwa kitabu cha Kutoka 31:12-18.

Pia kwa kitabu cha Walevi 26:1-12.

Na kwa kitabu cha Ukumbusho 5:12-63.

Na kitabu cha Isaya 55:1 hadi mwisho.

Vyote vinaongea kuhusu utukufu wa Siku ya MUNGU, siku ya Dimanche.

MUNGU awajalie baraka za kushika na kutukuza Siku ya MUNGU.

Tuilinde namna mwenye aliyetuumba anataka ilindwe.

Tutabarikiwa maisha yetu yote.

Amina. Amina.

Awalinde Muumba wetu. Awaongoze mwenye aliwaongoza wa Israeli kutoka Misri.

Awatoe kwa Misri zozote za magumu ya kiroho na ya kimwili.

Nyumba zenu zibarikiwe, na watoto wenu wabarikiwe, na kazi za mikono zenu zibarikiwe.

Na siku moja MUNGU muumba wetu awafikishe juu mbinguni penye tutakwenda kuishi na yeye milele na milele. Amina. Amina.

Mwaka Mpya wa baraka,

na miaka mingi mbele zijazwe na baraka vile.

Pious Ponsiano Kintu

4 December, 2018

Phone: WhatsApp +250 789 808857
Email: avemaria832@gmail.com
Website: www.avemaria832.simplesite.com